



REPUBLIC OF KENYA
COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI
SECOND ASSEMBLY –THIRD SESSION
THE HANSARD

Monday, 11th March 2019

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 2:30 p.m.*

[The Speaker (Hon. Kahindi) in the Chair]

PRAYERS

MOTION

PAPER LAID

THE COUNTY STRATEGY FISCAL PAPER 2019

Hon. Mwayaa: Thank you Mr. Speaker, Sir. I stand on behalf of the Leader of Majority and I wish to lay on the Table of this House the Kilifi County Fiscal Strategy Paper 2019. Thank you.

(Hon. Mwayaa laid the paper on the table)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you. Hon. Members the same is now committed to the respective committees and feedback to be availed to the House within fourteen days. Thank you.

STATEMENT

ORDER OF BUSINESS FOR THE WEEK COMMENCING 11TH MARCH 2019

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes Hon. (Ms.) Maneno.

Hon. (Ms.) Maneno: Thank you Mr. Speaker, Sir.

Pursuant to the provision of Standing Order 41 (2) (a), I wish to present and lay on the Table of this House the Statement regarding the Business of the House for the week commencing Monday 11th March 2019 as follows:-

Monday 2.30 p.m. that is today (A) Papers; The County Strategy Fiscal Paper 2019, which has already been done by the Majority Whip. A Motion by hon. Hadad Almasi for the Department of Gender, Culture, Social Services and Sports.

On Tuesday 9.30 a.m. that is 12th March 2019 we will have Papers. Report of the Sectoral Committee on Administration, Labour and Social Services on the petition made to the Kilifi County Assembly on the employment discrimination against privileged residents by the board of the Department of Health and Public Service Board. That will be done by the Chairman; Administration, Labour and Social Services.

The 2nd Quarter Report as from 1st October to 31st December, 2018 from the Department of Roads, Transport and Public Works. That will be done by the Leader of Majority.

On Tuesday 2.30 p.m. (A) Paper; 1) the 2nd Quarter Report as from 1st October to 31st December, 2018 from the Department of Agriculture, Livestock Development and Fisheries by the Leader of Majority.

The 2nd quarter report as from 1st October to 31st December, 2018 from the Department of Education and ICT by the Leader of Majority.

Wednesday 2.30 p.m. on 13th March 2019, (A) Paper 1), 2nd quarter report as from 1st October to 31st December, 2018 from the Department of Water, Forestry, Natural Resources and Solid Waste Management by the Leader of Majority. Thank you Mr. Speaker Sir.

MOTION

Hon. Hadad: Thank you Mr. Speaker, Sir. I beg to move the Motion to the CEC in charge of the Department of Gender, Sports, Youth, Culture and Social Services.

THAT, aware that Cultural activities, Public Entertainment and Amenities are devolved functions of the County Government as per the Second Schedule of the Constitution of Kenya 2010. Taking into account that the County Government of Kilifi has not held any Cultural festival since the inception of the county government.

Noting with concern that lack of their involvement has hindered the Mijikenda and other communities living within the county to showcase their unique traditional attire, songs, language and food which can promote our cultural heritage hence promoting domestic and international tourism.

This House urges the County Executive Committee in charge of the Department of Gender, Sports, Youth, Culture and Social Services and Trade, Tourism and Cooperative

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Development to come up with a county cultural festival making the event a success in the county. Thank you.

(Hon. (Ms) Nuzla seconded)

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you.

(Question proposed)

Hon. (Ms) Nuzla: Asante Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii. Mimi nimesimama kuunga mkono hii Hoja mia kwa mia. Mheshimiwa Spika tukikumba ya kwamba sisi hapa ndani ya Kilifi tuko na makabila mengi sana na makabila kama haya kutambulika ni kupitia zile tamaduni tulizo nazo. Lakini cha kushangaza ni kwamba huwa kaunti yetu huandaa tamasha lakini jambo la kusikitisha ni kuwa haijulikani hata kwa viongozi wetu na pia hata huwa vijana na jamii hawahusishwi ili kuonyesha utamaduni wao.

Mheshimiwa Spika, naomba tu nitoe mfano mmoja wa kaunti ambayo ni kaunti ndogo yenye maeneo bunge mawili ambayo ni Lamu. Tamasha za kuuza utamaduni wao unaofanyika katika kaunti hiyo ni kubwa sana. Kaunti ya Lamu ni sehemu ambayo ni ndogo na ina wananchi wachache lakini ukisikia tamasha yao ya utamaduni inayofanyika kila mwezi wa tisa ni tamasha kubwa ambayo huangaziwa na ulimwengu mzima na ni watu ambao ni wachache. Tamasha hii huhudhuriwa na mawaziri na hata maraisi kutoka nchi za nje ambapo hiyo huchangia uchumi ndani ya ile sehemu bila kuacha vijana kupata shughuli za kujiajiri wakati wa tamasha hiyo. Wakaazi pia vile vile wanapata kazi na pesa zinaingika ndani ya serikali hiyo na wananchi wanapata kufaidika.

Lakini ukiona huku kwetu ikifika tu wakati wa tamasha kama hizo hakuna vijana ambao wanahusishwa na hata kama kutakuwa na shirika ambalo hata limejitolea kujiunga na hiyo tamasha utaona pia serikali yetu haiungi mkono mia kwa mia. Utasikia mambo yanapangwa baadaye utaambiwa kuwa pesa hakuna na mambo mengine pia hakuna huku wananchi wa Kilifi pia vile vile huwa hawahusishwi.

Mimi ningeomba sisi kama wabunge tuunge mkono Hoja hii ili sisi kama wananchi wa Kilifi tuweze kufaidika na jambo kama hili pamoja na vijana kwa ujumla. Asante.

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you hon. (Ms) Nuzla. Yes Hon. (Ms) Elina Mbaru.

Hon. (Ms) Elina: Asante sana mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga mkono Hoja ambayo imeletwa na Mwenyekiti mdogo; tuliizungumzia kule Mombasa jinsi atakavyoileta hapa na leo ameileta ingawaje alikuwa anatafuta mtu wa kumuunga mkono na akawa amemchagua Mheshimiwa Nuzla. Basi wacha nimshukuru kwa kutimiza ahadi aliyoihidi kule Mombasa tulipokuwa na mkutano wa utamaduni. Tuliambia sasa ni wakati kama Idara watuletee hiyo *festival* huku Malindi kwa sababu kuna makabila mengi kama Bajuni na Mijikenda ili walete itikadi zao za kitamaduni. Kama alivyozungumzia Mheshimiwa Nuzla inapowekwa Kilifi inashikiliwa na makabila wengine wasiohusika. *Festival* iliyokuwa hapa mwaka jana kule Silversand ilishikiliwa sana na wakamba ambao sio watu wa hapa.

Tuliona tamaduni ambazo sisi kama wamijikenda hatujaziona; hatuhusishwi na hii *Department of Culture and Social Services*. Sasa tunaomba kwa yule anayehusika, waziri wetu wa *gender* ambaye tunamjua yeye ni mtenda kazi aje na mikakati ili mmijikenda wetu wa hapa ajue siku yake maalumu ya kutengeneza vitu vya kitamaduni. Hata sisi wa mijikenda tuko na utamaduni wetu lakini vile vinavyoendelea hapa ni vyakushangza; ule utamaduni wa kibajuni

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

hatuuoni na hapa watu wengi ni wa mijikenda na wabajuni. Tunaomba ule utamaduni unaofanyika Lamu na tushauona hauko mbali na wa wamijikenda hapa Kilifi. Ile iliyofanyika kule Silversand ilikuwa imehusishwa na mambo mengine sio ya kimijikenda. Tunataka kuhusisha wale wamijikenda wenyewe watuonyeshe utamaduni wao na wakaaji wa hapaa wajue siku yao ya mambo ya utamaduni.

Nimesimama kuunga mkono mwenyekiti mdogo wa kamati ya *Culture and Social Services* tuwe na mipangilio mizuri ya kutujulisha chakula hasa cha mijikenda ni gani? Mabajuni chakula chake kiko vipi? Ni ngoma gani ama ni utamaduni gani tulionao? Tuuelezee kwa maonyesho. Ninaunga mkono mambo ya *festival* yaletwe na ni njia moja ya kufanya *activities* hapa Kilifi ili wengine waje kuangalia utamaduni wetu.

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Hassan.

Hon. Hassan: Asante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nashukuru kwamba kamati ya tamaduni safari hii imefungukwa na macho na kutokwa na taka kwa masikio kwa sababu mimi binafsi limenikera kwa muda mrefu sana. Kama utakubaliana na mimi juzi tulikuwa na shughuli Kirinyaga na kwa bahati nzuri ikawa kila Kaunti inawakilishwa na vibanda vyao. Jambo lililonishangaza mimi pale kulikuwa na tamaduni za kipwani lakini kuna Bw. Mmoja aitwa Rotich yeye ndiye alikuwa anatuwakilisha sisi; amevaa zile nguo za kipwani, kwani tuko wapi ama twabebwa vipi? Naunga mkono hili donda liondoke tutambuliwe kama wengine.

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes hon. Baya.

Hon. Baya: Asante sana Mheshimiwa Spika. Nasimama kuunga mkono Hoja hii ikiwa imeletwa na mheshimiwa Hadad kama mwenyekiti mdogo katika Kamati ya Utamaduni na mimi pia nikiwa mwanakamati katika kamati hiyo. Mheshimiwa Spika ni muhimu sana kuwa na sherehe za utamaduni hapa Malindi. Juzi mimi na familia yangu tulikuwa ziara Zanzibar; nilienda kujionea haya mambo wenzetu wanatumia kama kitega uchumi. Tumeona hapa kwetu Kilifi tunavyo vitu vingi vinavyoweza kusaidia vijana wetu upande wa biashara ili kuondoa janga la ukosefu wa kazi. Naunga mkono mia kwa mia Mswaada huu ili upite.

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Maitha.

Hon. Maitha: Thank you Mr. Speaker. I rise in support of the Motion. Festivals act as stress relievers; when you attend a festival even if you are stressed that stress is relieved because of the activities going on there. Our tradition creates the foundation of our families; we have lost the critical part of our culture. Our founding forefathers had very rich culture due to civilization most of our culture is diminishing. Mr. Speaker I want to conquer with hon. Hassan. I was surprised too; our culture being represented by somebody who cannot at any point articulate the Mijikenda culture intensely.

We have heard the ban of disco matanga and there is a lot of resistance because we know very little about our culture. If we have a cultural festive in Kilifi County, I believe our youth will love the culture that we have as Mijikenda people. Mr. Speaker, our culture is diminishing; disco matanga is receiving a lot of resistance because we have no other place to turn to. If we have such a festival I believe our youth will love and have passion for our rich culture. I stand in support of the Motion.

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. (Ms) Mbuche.

Hon. (Ms.) Mbuche: Asante sana Mheshimiwa Spika. Naona Mheshimiwa Mbaru ananicheka sijui atarajia nini. Nimesimama kuunga mkono Hoja hii ya muhimu sana katika maisha yangu. Tulizungumzia kwa kina tulipokuwa kwa kamati kule Mombasa na tukasema wakati umefika kama kamati tuamke kwani mwaka uliisha hakukuwa na *entertainment* yoyote

kuhusiana na *culture, entertainment, talents and all this but...I am sorry* lakini Spika nakumbuka ...

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. (Ms.) Mbuhe I know you are very good in Kiswahili going by your programme Aziza so stick to Swahili please.

Hon. (Ms.) Mbuhe: Kile kimenifanya nichangie ni kwamba kuna mambo mengi mazuri Kilifi. Utamaduni sio kuonyesha mavazi na chakula pekee; kuna mambo mengi tuliyojaliwa nayo kama vipaji mbali mbali ambapo sherehe kama hii itakapokuwa tunaweza kualika kila mtu aliyebarikiwa na kipawa na ikawa ni uwanja mzuri wa kuonyesha talata mbali mbali ambazo ziko Kilifi. Kufikia sasa kuna tamaduni ambazo haziuziki katika ulimwengu huu na kuna zile tamaduni nzuri ambazo zinazuka kama vazi letu la kimijikenda bado laweza kuuzika. Kuna wale wanaoweza kulichambua vizuri kuanzia kichwa mpaka chini mimi nikiwa mmoja wapo; najua kulivaa na naweza kulieleza mpaka mtu akavutiwa na hizo shanga, mahando na vyakula mbali mbali kuna watu wanavitengeneza kama vile Mheshimiwa Elina alivyosema.

Tunaweza kuandaa chakula cha kitamaduni ambacho watoto wetu hawakijui lakini ni chakula ambacho ni kizuri hata wakila kikawa ni dawa kabisa katika maisha yao. Naunga mkono mia kwa mia ile Idara ihusishwe na kama hawawezi kuelewa tuwaelimishe na sheria itekelezwe. Mwezi wa nne unakuja wakati wa likizo watoto wako likizo, wazazi wamechukua livu tunaweza tukaandaa la sivyo mwezi wa nane ikiwezekana na Mwenyekiti na Naibu wako nataka mulivalie njuga jambo hili na sisi tuko nyuma kuchochea. Asante na Mungu awabariki.

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you. Hon. Mkadi.

Hon. Mkadi: Asante sana Mheshimiwa Spika kwa nafasi uliyonipa ili nami niweze kuunga mkono hoja hii. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu wa Kamati ambaye ameleta hoja hii mbele ya Nyumba hii. Sherehe hii huwa inasherehekewa sehemu mbali mbali na sisi kama watu wa Kilifi tumekosa nafasi kwa muda mrefu. Baada ya kujadiliana tunaona kwamba ni vyema sisi pia kupitia kwa Waziri wa Utamaduni aweze kupanga ili sherehe hii ifanyike hapa kwetu.

Ikifanyika italeti manufaa mengi ambayo yametajwa na wenzangu hapo awali lakini pia utamaduni kwa hasa sisi wamijikenda kwani kuna mambo mengi ambayo kwa sasa ndugu zetu hasa wadogo wamekosa kujua. Mengi ni kuhusiana na utamaduni ambao unafunza mambo ya kiduniani kwa sababu tuko na elimu ya dunia. Kwa hivyo sisi tumekosa hiyo nafasi ya kujua mambo yetu. Kama sisi wachonyi tuna taratibu zetu kama mvulana kuna umri akifikisha anachumbiana na msichana; taratibu zile kama tamasha zinaletwa hapa kwetu wengi wangepata nafasi ya kujieleza kujua ni tabia gani mtu anapaswa afanye jinsi wanavyofaa kujieleza. Mbali na hayo tungefanya mambo mengi ambayo yangeleta faida kwa Kaunti yetu. Kwa sasa yule atakayetegemea kufuata zile mila zetu na desturi hatungeita watu wachawi.

Zamani tulikuwa tukikosa mvua kwa muda mrefu kuna watu walikuwa wanajitolea na wanakijiji wanatoa vitu halafu wale wazee ambao wanajua zile mila wanaenda kwa sehemu fulani na kuomba mvua na mvua inanyesha ndio wakulima waendeleo na taratibu zao. Vile vile kama kumekuja ugonjwa ambao sio wa kawaida, kuna wazee ambao walikuwa wanaona kabla mambo yatokee na wanaenda sehemu ambazo zinafaa ili wafanye taratibu ya kimila na magonjwa yale hayatufikii. Lakini kwa sasa Kilifi Kaunti haijapewa nafasi labda ya kuonyesha yale mambo kuhusu mila zetu. Inakuwa ni shida mambo mengi ambayo labda yanaleta faida hayawezekani. Nasimama kuunga mkono Hoja hii na wenzangu pia waunge ili tuweze kushuhudia mila zetu hapa. Asante Bw. Spika kwa nafasi hii.

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you for your contribution.

(Question, that the Mover be now called upon to reply, put and agreed to)

Hon. Hadad: Thank you Mr. Speaker and I would like to quote the importance of culture in the Constitution. Chapter 2 of the Constitution of Kenya states that;

“The Constitution recognizes culture as the foundation of the Nation and as the cumulative civilization of the Kenyan people and Nation. The State shall promote all forms of national and cultural expression through literature, the arts, traditional celebrations, science, communication, information, mass media, publication, libraries and other cultural heritage”.

Mr. Speaker, we have good examples within Kenya of Counties which benefit from culture. We have Narok County; more than 50% of the income comes from cultural festivals. We also have Lamu and these have benefited a lot. Before in Kilifi we used to top when it comes to tourism but what happened? Our tourism industry collapsed and it is because we forgot our culture. We forgot our foundation and also where we were coming from but once we revive our culture then we will have a lot in this county.

Mr. Speaker; His Excellency the Governor Hon. Kingi launched this is Kilifi platform. Kilifi has been marked as a tourism attraction and we have nothing to showcase. What is the reason behind it? We are wasting our time and whatever we do we must have a follow up to add weight on it. This is an importance chance to make this application relevant to the people. It will also attract tourists to this county. Once our tourism industry is improved, many youth will be employed and poverty level will reduce. Many problems will be solved.

We have early childhood pregnancies; all this will be a thing of the past if we go back to our culture. Mr. Speaker, I really appreciate all the hon. Members for supporting this Motion. Thank you.

(Question put and agreed to)

The Speaker (Hon. Kahindi): Just before we conclude my advice on this Motion; this is a very important Motion and if you ever asked yourself why the festival in Lamu is usually held in September, it is simply because there is a budgeting process that comes rightly before it. If you want to see the success of this Motion, as the Chairperson of the Culture Committee, make sure you allocate money for that festival otherwise you will have passed a very beautiful Motion with very good content but implementation will not be possible.

This has been tried before but you see when there is no money that has been attached to it, the CEC Member cannot do anything. So hon. Hadad we are in the process of engaging in the budget making process. Right now the Executive cannot implement this unless in the budget your committee sets aside some money that will jumpstart the process and that is why I have also done research why Lamu always have it around September.

The County Government must pump money to advertise, market and prepare the venue; you know when it is taken over by Government then it becomes something substantive. As Kilifi we have been putting it under private companies like Mseto Africa which ultimately then we do not see the results. It is a good Motion and I think in my view that is the direction that needs to be taken.

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

MEETING OF CHAIRPERSONS AND VICE CHAIRPERSONS

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Before we adjourn I am informed that Chairpersons and Vice Chairpersons are required to stay behind so that they can be given the programme of the just laid County Fiscal Strategy Paper.

ADJOURNMENT

In the absence of any other business to transact, I move to adjourn this Sitting until tomorrow. Thank you very much.

The House rose at 3:00 p.m.